



**HADHRAT MIRZA GHULAM AHMAD (a.s.)**  
*Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa*

**BAADHI  
YA  
MAANDIKO**

**YA**

**HADHRAT AHMAD (A.S.)**

**Mfasiri  
ATHUMANI M. GAKURIA**

**Kimeenezwa na:  
AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT  
P.O. Box 40554, Nairobi, Kenya  
East Africa**

**Baadhi ya Maandiko ya Hadhrat Ahmad (a.s.)**

**Haki zote zimehifadhiwa**

**Chapa ya Kwanza 1989 Nakala 3,000**

**Chapa ya Pili 2009 Nakala 2,500**

**Kimechapishwa na Ahmadiyya Printing Press  
P. O. Box 376  
Dar es Salaam  
Tanzania**

**ISBN 9987 - 438 - 05 - 9**

# **YALIYOMO**

<b>Utangulizi</b> .. . . . .	<b>v</b>
<b>Allah Mtukuka</b> .. . . . .	<b>1</b>
<b>Kudhihiri kwa Mwenyezi Mungu</b> .. . . . .	<b>2</b>
<b>Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w.)</b> .. . . . .	<b>6</b>
<b>Ujaji wa Masihi Aliyahidiwa (a.s.)</b> .. . . . .	<b>9</b>
<b>Shabaha za Kuanzishwa Jumuiya ya Waislamu</b>	
<b>Waahmadiyya</b> .. . . . .	<b>11</b>
<b>Kuwasingizia Wengine</b> .. . . . .	<b>15</b>
<b>Wahyi</b> .. . . . .	<b>17</b>
<b>Malaika</b> .. . . . .	<b>19</b>
<b>Kujitahidi Katika Njia ya Mwenyezi Mungu</b> .. . . . .	<b>21</b>
<b>Maombi</b> .. . . . .	<b>23</b>
<b>Imani Zetu</b> .. . . . .	<b>24</b>
<b>Dhambi</b> .. . . . .	<b>25</b>
<b>Wokovu</b> .. . . . .	<b>26</b>
<b>Maisha Baada ya Kifo</b> .. . . . .	<b>27</b>
<b>Roho</b> .. . . . .	<b>28</b>
<b>Hakika ya Yajuja na Majuja</b> .. . . . .	<b>29</b>
<b>Msimu wa Mwangaza</b> .. . . . .	<b>30</b>
<b>Kurani Tukufu</b> .. . . . .	<b>32</b>
<b>Dini za Dunia</b> .. . . . .	<b>36</b>
<b>Huruma kwa Wanadamu</b> .. . . . .	<b>37</b>
<b>Hali ya Baadaye ya Ahmadiyyat</b> .. . . . .	<b>38</b>
<b>Hatimaye Ushindi</b> .. . . . .	<b>39</b>

# **BAADHI YA MAANDIKO YA HADHRAT AHMAD (A.S.)**

## **MASIH NA MAHDI ALIYEAHIDIWA**

Katika kusherehekeea Karne ya Jumuiya ya Kimataifa ya Waislamu Waahmadiyya

Hii ni zawadi toka kwao hao Waislamu Waahmadiyya, ambao hata katika zama hizi, wanataabishwa na kuuawa kwa sababu hii tu kwamba wao wanapenda na wanatangaza Umoja wa Mwenyezi Mungu. Wao ndio mfano ulio hai wa imani thabiti ya Hadhrat Bilal r.a. \*

---

\*Hadhrat Bilal (Mungu Awe radhi naye) alikuwa mmoja wa Masahaba wa Mtume Mtukufu Muhammad (S.A.W.). Licha ya kuteswa vikali kwa sababu ya kusilimu, yeze akawa tayari kufa kuliko kuukana Umoja wa Mwenyezi Mungu.

## **UTANGULIZI**

Sasa imetimia miaka mia moja tangu Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (1835-1908) atangaze kwamba ye ye alikuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Kutangazwa kwa baadhi ya mafundisho yake kunafanyika kama sehemu ya mpango wa kuadhimisha Karne ya Jumuiya, ambayo ni jamii ya Waislamu iliyoanzishwa na Mungu Mwenyewe.

Licha ya upingamizi na uadui, Jumuiya imeendelea kusitawi kwa haraka pande zote za dunia. Tayari Jumuiya imezagaa katika nchi 120 na yazidi kusonga mbele ikiwa ndiyo sauti halisi ya Islam.

Njia bora zaidi ya kuelewa ujumbe, uzani na mipango ya Ahmadiyyat ni kujaribu kuyaelewa madai yaliyofanywa na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s.). Mbinu yenye uhakika na njia yenye busara ndiyo kujaribu kuyajibu kiadilifu maswali yazukayo akilini mwa mtafuta haki kutokana na maandiko ya yule mtu mwenyewe aliyedai kuwa ndiye Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa.

Hapa yapo baadhi ya maneno yaliyonukuliwa toka maandiko yake - maneno ya kawaida na tenzi pia - zenye kueleza shughuli mbali mbali za kibinadamu. Twatumaini ya kwamba msomaji sio kwamba atajifunza mengi tu bali pia atagundua ukweli kwamba kutalii kijitabu hiki ambacho ni kifungua milango ya vitabu zaidi ya 80 alivyoviandika, kuwa pia kватia nuru moyoni kwa njia nyingi.

Tafsiri hii ya Kiswahili imetokana na ile ya Kiingereza na uangalifu mwingu umetumiwa ili kuhifadhi maana zote za maneno ya asili.

Jumuiya ya Kimataifa ya Waislamu Waahmadiyya, ilianzishwa hapo mwaka wa 1889 katika kijiji cha Qadian nchini India. Mwanzilishi wake, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s.) alidai kuwa ye ye ndiye yule Kiongozi Aliyeahidiwa ambaye ujali wake ulikuwa ukibashiriwa kwa majina mbali mbali na wafuasi wa dini mbali mbali. Mabaniani walimsubiri Krishna; Wakristo walingojea Masiha: wafuasi wa Budha walimsubiri Budha mwenyewe, ilahi Waislamu walimngojea Mahdi na Masihi pia.

Kwa amri ya Mwenyezi Mungu, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s.) akatoa tangazo lisilotazamiwa ya kuwa kumbe alikuwa aje Kiongozi mmoja tu kuwakilisha viongozi waahidiwa hao wote na jukumu lake lilikuwa hatimaye kuwakusanya wanadamu wote chini ya kivuli cha dini moja ya ulimwengu mzima. Isitoshe, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s.) akasisitiza ya kwamba huyo Kiongozi Mwahidiwa asingekuja na cheo cha kujitegemea ila kama mfuasi wa Mtume Mtukufu tu wa Islam Hadhrat Muhammad Mustafa (S.A.W.). Aliiamini Islam kuwa ndiyo sheria timilifu na ya mwisho kwa ajili ya wanadamu wote, ndipo madai yake kwamba yule Kiongozi aliyekuwa akingojewa ilikuwa lazima kudhiihiri katika Islam

akiwa Nabii mfuasi wa Hadhrat Muhammad (S.A.W.). Akatangaza akisema kwamba ujaji wake mwishowe utaananza zama tukufu za kuwepo kwa dini moja tu kwa ajili ya wanadamu wote, zama ambazo mwanadamu daima amezitamani na kuzisubiri.

Katika mwaka wa 1889 akaamriwa na Mwenyezi Mungu kuweka msingi wa Jumuiya itakayofanikisha malengo na shabaha za ujaji wake. Ndipo hapo tarehe 23 Machi, mwaka wa 1889 akatangaza rasmi kuanzishwa kwa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwa kuchukua ahadi ya Baiati ya wale walioamini madai yake, alipokuwa mjini Ludhiana, mkoani Punjab nchini India.

Tangu kuzalika taifa la Pakistan, Waislamu wengi pamwe na Kiongozi wa Jumuiya kuhamia Pakistan, Makao Makuu ya Jumuiya yalihamishwa Pakistan katika mji mdogo wa Rabwah uliojengwa na Jumuiya.

Mara kwa mara wapinzani wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya wamezusha ghasia nydingi dhidi ya Waahmadiyya. Mionganoni mwao zile ghasia za miaka ya 1953, 1974 na 1984 zafahamika sana. Njama na ghasia za mwaka wa 1984 dhidi ya Ahmadiyyat zikapata kibali na msukumo kamili wa Serikali ya Pakistan na tangu iundwe sheria dhidi ya Ahmadiyyat, vikwazo vikali vya aliyekuwa kiongozi wa Pakistan marehemu Jenarali Zia ul Haq vyabana na kuyakwamisha maendeleo ya Jumuiya na kuwanyima Waahmadiyya wa Pakistan haki zao zote za kibinadamu.

Ingawaje, Jumuiya imeteseka vikali, njama za Serikali na masheikh kwa msaada wa Mwenyezi Mungu hazikufua dafu nchini Pakistan.

Ama kuhusu sehemu zingine za dunia, kama matokeo ya upinzani, Waahmadiyya wamepata ikhlasi zaidi na moyo mpya, jambo ambalo limeharakisha mno maendeleo ya Jumuiya.

Hata hivyo, kwenye juhudhi hizi za kufa na kupona na kupigania haki za kibinadamu, maelfu ya Waahmadiyya wamepata mateso makali pamoa na kutupwa gerezani, kupigwa na hata kuuawa kinyama.

Mionganoni mwa sherehe za kutoa shukurani katika mwaka wa 1989 wa maadhimisho ya Karne, jambo la shukurani kubwa zaidi kwa Mola wa huruma, litatekelezwa kwa njia ya kuchapisha tafsiri za Kurani Tukufu, Hadithi za Mtume Mtukufu (S.A.W.) na baadhi ya Maandiko ya Mashih Aliyeahidiwa katika lugha zaidi ya mia moja. Kijitabu hiki ni sehemu ya utekelezaji wa mpango huu mkubwa uliojaa baraka.

**S. H. ABBASI,  
Add. Vakilut Tasneef  
and Nazir Ishaat  
London.**

## ALLAH MTUKUKA

Hakika pepo yetu ni Mungu wetu na ladha yetu yote ni kwa Mola wetu. Sababu, sisi tumemwona na tumeukuta kila uzuri ndani Yake. Inafaa kujipatia hazina hii hata kwa kutoa roho. Na inafaa kununua almasi hii hata kwa kutoa uhai wote. Enyi wenyе bahati ndogo kimbilieni upesi kwenye chemchem hii ambayo itatuliza kiu yenu. Ndiyo chemchem ya uzima itakayowalindeni. Nifanye nini, na niingize namna gani miyoni mwenu maneno haya ya furaha? Kwa ngoma gani ninadi katika masoko kuwa Mola wenu ni Huyu ili watu wasikie? Na niwape tiba gani ili masikio ya watu yafunguke na yasikie?

(*Roohani Khazain Jal. 19: Safina ya Nuhu uk. 15*

Sikilizeni enyi mlionna masikio: Ni jambo gani Alitakalo kwenu Mwenyezi Mungu? Ni hili tu kwamba muwe Wake Yeye pekee wala msimshirikishe na cho chote, iwe hapa duniani au huko mbinguni. Mungu Wetu ndiye Yule Aliye hai; tena Yeye Yuwaongea leo hii kama Aliviyodumu kuongea tangu kale; Yuwasikia kama Aliviyodumu kusikia tangu azali. Ni imani mbovu kudhani kwamba Yeye leo hii husikia tu, lakini Haongei. Naam, Yeye Yuwasikia na kuongea pia. Sifa Zake zote ni za azali na za milele. Hapana sifa yake moja iliyopata kukatizwa au itakayopata kukatizwa. Ni Dhati Yule Yule pekee Asiye na mshirika; Hana mwana wala mke; na ni Dhati Yule Yule wa milele Asiye na kifani, na hapana afananaye naye; hapana aliye na sifa kama Zake; hapana uwezo Wake unaoweza kufifia. Yu karibu ilhali Yu mbali, tena Yu mbali ilhali Yu karibu ... Yeye Yu juu ya walio juu, lakini haiwezekani ikasemwa kwamba pana ye yote chini yake aliye mbali kumshinda yeye. Yeye Yu mbinguni, lakini haiwezi kusemwa kwamba Hayupo ardhini. Amejikusanya Kwake sifa zote njema, na Hudhihirisha utukufu ule ambao kwa hakika wastahili kusifika; Yeye ndiye chanzo cha utukufu wote; Yeye ndiye mwenye uwezo wote. Kila jambo jema huanzia Kwake na kila jambo hurejea Kwake; ni Zake hazina zote, utukufu wote umekusanyika katika Dhati Yake. Hana kasoro yo yote, wala udhaifu. Ni wa pekee katika haki yake ya kuabudiwa na wote waliomo ardhini na wale wa mbinguni.

(*Roohani Khazain Jal. 20: Al-Wasiyyat uk. 10-11*

## KUDHIHIRI KWA MWENYEZI MUNGU

Asiyeepukana na tashwishi hawezi kuepukana na adhabu. Mkosa bahati akosaye kudhihirikiwa na Mungu humu duniani hata huko Akhera atakuwa gizani. Mwenyezi Mungu asema:

مَنْ كَانَ فِي هُدَىٰ أَعْلَمُ فَهُوَ فِي الْآخِرَةِ أَعْلَمُ

“Na aliye kipofu katika (dunia) hii, basi atakuwa kipofu katika Akhera” (17:73).

(*Roohani Khazain Jal. 13: Kitab-ul-bariyya uk. 47.*)

Naam, Mweza wa yote na Mwenye nguvu ni yule Mungu Ambaye Waumini Wake hawatahasirika kamwe; wale wamjiao kwa mapenzi na uaminifu. Adui hujigamba kwamba atawaangamiza wote kwa ushetani wake na mwenye nia mbaya huapa kwamba atawamaliza. Wapumbavu ninyi, Asema Mwenyezi Mungu, je, mtajasiri kupigana nami? Na kumdhahilisha yule aliye mpenzi wangu? Kwa hakika, lolote haliwezi kuikumba dunia hii ila liwe limekadiriba hivyo huko mbinguni, wala hakuna mkono wa kidunia uwezao kufikisha dhoruba zake nje ya eneo ulilopimiwa huko mbinguni. Hivyo basi, wenyewe kula njama za uovu na ukatili ni wapumbavu mno ambao katika harakati za mipango yao miovu ya aibu, hawamkulabi Yule Dhati Mkuu Ambaye hata jani haliruhusiwi kudondoka bila ya amri Yake. Kwa hivyo, wao huibuka na kushindwa na shabaha zao kutotimia; wala njama zao haziwadhuru wale walioongoka; kinyume chake ishara za Mungu huenea zaidi na fahamu za watu juu ya kudra ya Mwenyezi Mungu huongezeka. Yule Mungu Mweza, Mwenye nguvu, Asiyeonekana kwa macho, Hujidhihirisha kwa hakika kupitia kudra Zake za ajabu.

(*Roohani Khazain Jal. 13: uk. 19: Kitab-ul-bariyya, Muqaddama uk. 1*)

Mwenyezi Mungu Ndiye nuru ya mbingu na ardhi. Kila nuru ionekanayo, iwe juu au chini, iwe yatokana na roho au miili, iwe ya kikhulka au ya kuazima, iwe iliyofichana au wazi, iwe yenye kutiisha ama kutiishwa,

ndio ukarimu wa neema Zake. Hii ni ishara imaanishayo kwamba ukarimu wa Mwenyezi Mungu unakifunikiza kila kitu. Yeye ndiye chemchem ya baraka zote na ndiye chanzo cha asili ya kila nuru, chemchem ya rehema zote. Dhati yake ndiyo mlezi wa ulimwengu wote na ndilo kimbilio la wote wakubwa kwa wadogo. Ni Yeye Aliyekichomoza kila kitu toka giza la kutokuwepo kwao na Akakijaalia kila kitu kuwepo. Hapana ye yote minghairi Yake aliyepo kwa kujitegemea ama aliye wa milele; kila aliyepo ni mpokeaji wa baraka Zake. Ardhi na mbingu, watu na wanyama, mawe na miti, roho na miili, vyote Anavilea Yeye.

(*Roohani Khazain Jal. 1, Maelezo Uk. 191-192: Braheen-e-Ahmadiyya, Maelezo 11*).

Sifa zote njema ni Zake Yeye Aliye wa milele. Hapana aliye sawa naye, wala hapana afananaye naye. Anadumu milele, vingine vina mwisho. Kuwapenda wengine kuliko Yeye ni ndoto tu. Yeye tu ndiye tumaini la moyo wangu, simjui mwengine. Moyo wangu wanadi: Yu Mtakatifu Yeye Anilindaye. Anawalea wote, baraka Zake zi wazi. Kwake tu twapata utulivu; Yeye tu ndiye mpenzi wetu. Hatuwezi kuishi bila Yeye, vingine vyote ni bandia. Ibarikiwe siku hii, Yu Mtakatifu Yeye Anilindaye.

(*Roohani Khazain Jal. 12, Uk. 319: Mahmud Ki Amin Uk. 3*).

Mimi nasema kweli kwa hakika kama roho zina hamu ya kutafuta na nyoyo kupata shauku ya elimu, basi hapo wanadamu watapata jazba ya kugundua mwanga ule na Njia ile. Lakini mtu auezaje kuifikia Njia ile na macho yatafumbuliwa namna gani? Nawahakikishia wale wote watafutao ya kuwa ni Islam pekee itoayo habari njema za njia ile. Dini zingine zilishauziba mlango wa wahyi wa Mungu tangu zamani za kale. Hivyo, jueni kwa yakini kwamba si Mwenyezi Mungu Aliyeukwamisha ufunuo. Bali ni mwanadamu, ili kuhalalisha kunyimwa kwake, yeye anafuta kujibanza kwenye kisingizio hiki. Fahamuni wazi (kabisa) kwamba kama vile isivyowezekana kuona pasina macho au kusikia bila masikio au kuongea bila ya ulimi, vivyo hivyo ndivyo isivyowezekana kumwona Mwenyezi Mungu wetu, Mpendwa, bila

Kurani Tukufu. Nilikuwa kijana. Sasa nimezeeka. Lakini sikumwona ye yote ambaye, pasina chemchem hii safi ya Kurani Tukufu, akajaaliwa kunywa toka kikombe cha mwongozo ulio safi ujidhihirishao.  
*(Roohani Khazain Jal. 1, Maelezo Uk. 191-192).*

- (i) I wazi kiasi gani nuru ya Mwenyezi Mungu Aliye chanzo cha nuru zote. Ulimwengu wote wageuka kuwa kioo cha kuyawezesha macho kumwona.
- (ii) Jana usiku nilipoutazama Mwezi, nikapata mahangaiko. Ndani ya uzuri wa Mwezi ulikuwemo uzuri wa Mungu Mpendwa.
- (iii) Kwa athari ya mchanganyiko uzuri ule moyo wangu wahangaika; usinitajie uzuri wa Mturuki au mtu wa Tatari.
- (iv) E wangu Mpandwa! Ni kwa njia ya ajabu ulioje uwezo Wako wa kuumba udhihirishwavyo kote kote.  
Kila nitazamako, nakuta kila njia yaelekeea Uliko Wewe.
- (v) Ndani ya kivimbe cha Jua, mawimbi ya uwezo Wako yashuhudiwa; kila nyota yameta meta kwa adhama Yako.
- (vi) Kwa mkono Wako Mwenyewe umezimwagilia chumvi nyoyo zenye hima; matokeo yakiwa kupaazwa kwa sauti za wapendanao.
- (vii) Ni khulka za ajabu kiasi gani ulizoijsaalil kila chembe.  
Ni nani mwenye elimu ya kuyazunguka maajabu haya yote?
- (viii) Hapana aezaye kuizunguka hatima ya shabaha ya uumbaji Wako. Ni nani aezaye kutanzua siri za kitendawili hiki?
- (ix) Ni uzuri Wako ulio kiini cha kila uzuri. Kila ua lichanualo huazima rangi yake toka kwa fahari ya sifa Zako.

- (x) Uzuri wa macho ya wale waliojaliwa uzuri wamfanya mtu kukumbuka kila dakika. Kila kishungi kilichokunjanakunjana chakunyooshea kildole.

(*Roohani Khazain Jal. 11 Uk. 52: Surma Chashm-e-Arya Uk. 4: Beti za Shairi “Kasida kwa Mwenyezi Mungu”*).

Umoja wa Mungu ni nuru iuangazao moyo baada ya kukatalia mbali miungu yote, iwe ni miungu ya dunia ya ndani au dunia ya nje. Huifunikiza kila chembe ya nafsi ya mtu. Hali hii yawezaje kupatikana bila msaada wa Mwenyezi Mungu na kumfuata Mtume Wake? Wajibu wa mtu ni kujua nafsi yake na kuyapa kisogo majivuno ya kishetani. Asijigambe eti ameletelewa kwenye kao la elimu, bali yuwapaswa kujihesabu kuwa mtu asiyejua cho chote, na kudumu katika maombi. Ndipo nuru ya Umoja wa Mungu itamshukia na kumpatia maisha mapya.

(*Rhoohani Kazain Jal. 22, Uk. 148: Hakikatul - Wahyi Uk. 144*).

## **MTUME MTUKUFU MUHAMMAD (S.A.W.)**

Nuru tukufu aliyojaaliwa mtu yaani yule mtimilifu zaidi mionganini mwao, haikugawiwa malaika, wala nyota, wala haikuwemo mwezini au juani, au katika bahari na mito; haikuwa ipatikane katika vitu vya zumaradi au lulu n.k.; haikuwemo katika kitu cho chote cha ardhini au mbinguni. Nuru hii alikuwa nayo mtu mkamilifu peke yake, ikadhihirika kwa njia timilifu kabisa katika dhati ya Bwana wetu na Kiongozi wetu, Muhammad Mtukufu, mbora wa Manabii wote, kiongozi wa wale walio hai (machoni pa Mungu). Hivyo basi, ile nuru tukufu akaipata mtu yule kikamilifu kabisa, na vivyo hivyo, kwa kiasi fulani, wakapewa wale wote ambaao katika baadhi ya hali zao, walifanana naye .... Neema tukufu katika dhihirisho lake timilifu zaidi akaipata Bwana wetu na Kiongozi wetu, Nabii asomjuzi wa kusoma wala kuandika, mkweli, ambaye uaminifu wake washuhudiwa, Muhammad mteule, amani na baraka za Mwenyezi Mungu juu yake.

*(Roohani Khazain Jal. 5, Uk. 160-162: Aaina Kamalat-e-Islam Uk. 160).*

Daima namstaajabia sana Nabii huyu Mwarabu, aitwaye Muhammad, maelfu ya baraka na amani viwe juu yake. Cheo chake kilinyanyuka kiasi gani! Mtu hawezi kukisia upeo wa mwisho wa daraja yake, wala si kazi ya binadamu kufahamu vina na undani wa athari ya khulka zake zitukuzazo. Kumbe daraja yake iliyonyanyuka sana haikufahamika vyema. Ule Umoja wa Mungu ambaao tayari ulikuwa umetoweka juu ya uso wa ardhi ukapandwa upya na huyu huyu mshindi wa washindi. Alimpenda Mwenyezi Mungu kupindukia, na ndivyo moyo wake ulivyoyeyuka kwa kuwahurumia wanadamu. Ndio maana Mwenyezi Mungu, Aliyejua sana ubora uliofichana moyoni mwake, Akamnyanya kuliko Manabii wote na watu wote wa zamani na wale watakaokuja nyumaye, na Akamtizimia matumaini ya moyo wake katika maisha yake.

*(Roohani Khazain Jal. 22: Hakikatut-Wahyi Uk. 115-116).*

Mtume wetu Mtukufu, (S.A.W.) amekusanya katika dhati yake majina ya Manabii wote, kwani katika dhati yake zimekusanyika khulka bora tanazozipata mara kadhaa katika dhati za Manabii wengine wote. Ndipo yeye ni Musa na Isa pia; yeye ni Adam na ni Ibrahim, yeye ni Yusuf na Yakub pia. Mwenyezi Mungu Anadokeza ukweli huu katika aya:

فِي هُدًى مُّبِينٍ

Yaani: Basi ufuate mwongozo wao. (6:91).

Maana yake: E Nabii wa Mungu, jikusanyie mafundisho mbali mbali ya manabii. Hii inamaanisha kwamba utukufu wa manabii wote ulikusanywa katika dhati ya Mtume Mtukufu (S.A.W.). Ama kwa hakika jina lenyewe Muhammad ladekeza ukweli wenyewe kwa sababu lina maana ya “Asifiwaye sana”. Sifa tukufu zaidi yaweza kuwazika pale tu inapokubalika kwamba khulka na sifa za Manabii wote zimekusanywa katika dhati yake.

(*Roohani Khazain Jal. 5: Aaina Kamalat-e-Islam, Uk. 343*).

Nimejulishwa ya kwamba mionganini mwa Manabii wote, yule aliyefikisha mafundisho matimilifu na safi yaliyojaa busara na yule aliyeonyesha nafsini mwake khulka bora zaidi za kiutu ndiye Mtume Mtukufu Muhammad, Bwana na Kiongozi wetu, amani na baraka za Mungu ziwe juu yake.

(*Roohani Khazain Jal. 17: Arbaeen No.1 Uk. 3*)

Tuchunguzapo kwa roho safi bila mapendeleo Manabii wote wa zamani, twapata ya kwamba Hadhrat Muhammad Mtume Mtukufu wa Islam (S.A.W.) ndiye shujaa kupita wote, ndiye aliyekusanya sifa zote za maisha na ndiye aliyempenda Mwenyezi Mungu zaidi.

(*Roohani Khazain Jal. 12: Siraj-e-Muneer Uk. 72*)

Tukio la ajabu lilitukia kwenye majangwa ya Arabia, ambapo mamia ya maelfu ya wafu yakafufuka katika muda wa siku chache, na wale

ambao walikuwa mafasiki kwa vizazi vingi wakavaa vazi la ucha-Mungu. Vipofu wakaanza kuona, na ndimi za mabubu zikaanza kububujisha elimu za Kiungu. Ikatokea aina ya mapinduzi duniani ambayo hapana jicho lililokuwa limepata kushuhudia wala sikio lililokuwa limepata kusikia mfano wake. Je, mwajua hicho kilikuwa kitu gani? Hayo yote yalisababishwa na maombi ya usiku ya mtu aliyekuwa amejipoteza kabisa kwa Mwenyezi Mungu yaliyoleta mwamko duniani na kudhihirisha maajabu yasiyoaminika kwamba yangeweza kuletwa kwa mkono wa mnyonge yule asiyejua kusoma wala kuandika. E Mwenyezi Mungu! Mteremshie baraka Zako ye ye waifuasi wake kadri ya mahangaiko na uchungu aliokuwa nao juu ya Ummah wa Kiislamu, na umfikishie nuru ya neema Zako daima dawamu.

*(Roohani Khozain Jal. 6: Barakatud Dua Uk. 10).*

## UJAJI WA MASIHI ALIYEAHIDIWA (A.S.)

Katika ruya mimi nikaona kwamba watu walikuwa wakitafuta Mujaddid. Mmoja wa watu hao akajitokeza mbele na huku akininyooshea kidole, akatangaza akisema, "Huyu ndiye mtu ampendaye Mtume wa Mungu". Kwa maneno haya wao walimaanisha alama kubwa ambayo Mujaddid ajaye ni sharti awe nayo ilikuwa mapenzi yake juu ya Mtume Mtukufu (S.A.W.) na sawa na rai yao sharti hili mimi nilikuwa nimelitimiza barabara.

(*Roohani Kazain Jal. 1, Uk. 528 maelezo ya ziada: Braheen-e-Ahmadiyya*)

Ulimwengu hauwezi kunikubali, kwani mimi sitokani na ulimwengu huu. Lakini wale waliojaaliwa vipawa vya dunia nyingine ndio wanaonikubali, na watanikubali. Anikataaye anamkataa Yeye Aliyenituma na anayepandikizwa kwangu mimi basi amepandikizwa kwa yule ninayemwakilisha. Mimi ninao mwenge utakaowaangazia wote watakanisogelea. Lakini mwenye kughafilika kwa tashwishi na kukimbia ataingia gizani. Mimi ndimi ngome isiyoparamika kwa ajili ya zama hizi; ye yote aunganaye na kundi langu atapata salama dhidi ya wezi, wanyang'anyi na wanyama wa mwituni.

(*Rhoohani Khazain Jal. 3 Uk. 34: Fath-e-Islam Uk. 34*).

Naapa kwa Mwenyezi Mungu Mweza, Mwenye uhai wangu mikononi Mwake, kwamba kulinganisha na kila roho, mimi Amenijaalia uwezo mkubwa na Amenifungulia mlango ufikishao kwenye vina vya ndani vya hekima ya Kurani Tukufu. Kama ye yote mionganoni mwa masheikh wanipingao katika kuitikia mwito wangu wa mara kwa mara angelikuwa amejaribu kunikoga katika ubora wa maelezo ya Kurani Tukufu, bila shaka Mwenyezi Mungu Angelibatilisha jithhada zake na kubanisha ujinga wake. Ndipo sasa, ujuzi wa Kurani Tukufu niliojaaliwa ni ishara ya Allah, Mwenye adhama, nami nina tumaini la hakika juu ya rehemza Allah ya kwamba hivi karibuni dunia itaanza kutambua ya kuwa mimi ni mkweli katika madai yangu haya.

(*Roohani Khazain Jal. 2 Uk. 41: Siraj-e-Muneer Uk. 41*)

Mimi siko peke yangu. Mola Mtukufu yu pamoja nami. Hapana awezaye kuwa karibu nami zaidi Yake. Ni kwa rehema Zake tu kwamba mimi nimejaaliwa roho ya upendo, daima iko tayari kutumika katika njia Yake licha ya dhiki kubwa; ili nitoe huduma bora zaidi kwa jazba na uaminifu kwa ajili ya dini Yake na kuipatia Islam ushidi katika uwanja wa vita vya kiroho. Yeye Amenituma kutekeleza wajibu huu, na hapana awezaye kunifanya nijizui nisihitimishe jukumu hili.

(*Rhoohani Khazain Jal. 5 Uk. 35: Aaina-e-Kamalat-e-Islam* Uk. 35).

Igekuwa hoja tosha kwa mtu mtawa kuona kwamba Mungu Alinishushia baraka za nje na ndani, juu ya mwili wangu na roho nisizoweza kuhesabu. Nilikuwa kijana zama nilipodai kuwa mpokeaji wa wahyi wa Mungu. Sasa nimezeeka. Miaka zaidi ya ishirini imepita tangu mwanzo wa madai yangu. Marafiki zangu wengi wachanga kunishinda wamefariki, lakini Yeye Amenijaalia huu umri mpevu. Amedumu kuwa Mwongozi wangu na Yeye pekee Alitosha kuniondolea vizingiti vyote. Hebu niambieni, je, hizi ni alama za wale wamzuliao uwongo Mwenyezi Mungu?

(*Rhoohani Kazain Jal. 11 Uk. 50: Anjam-e-Atham*).

## **SHABAHA ZA KUANZISHWA JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA**

Enyi marafiki zangu mlionfanya maagano nami, Mungu Aniwezeshe na Awawezesheni kutenda yale yatakayompendeza Yeye. Leo hii ninyi ni wachache katika idadi. Mnapita katika kipindi chenye majaribio makubwa. Sawa na kanuni Zake za azali, ilikwisha ridhiwa na Mwenyezi Mungu tangu kale kwamba juhudzi zitafanywa toka kila upande ili ninyi mteleze. Mtasumbuliwa kwa kila njia, nanyi mtalazimika kuvumilia matamshi ya kila aina. Kila mmoja wa wale watakaowataabisheni kwa ulimi wake ama kwa mkono wake, atafanya hivyo akiamini kwamba anaihudumia Islam. Hali kadhalika, mtatahiniwa mbinguni ili kwamba muwe mmetahiniwa kwa kila njia iwezekanavyo. Fahamuni kwa hivyo, ya kwamba njia ya ushindi kwa ajili yenu haielekei kwenye hoja kame mtakazotumia au kwamba ninyi muwazomee wanaowazomeeni au kwamba myajibu matusi kwa matusi. Mkitumia mbinu hizi nyoyo zenu zitakuwa kavu nanyi hamtabaki na cho chote ila maneno matupu ambayo Mwenyezi Mungu Anayachukia na kuyabeza. Hivyo basi, msishike tabia ambayo kwayo zitahakiki juu yenu laana mbili - laana ya watu na laana ya Mungu.

*(Roohani Khazain Jal. 3 Uk. 546-548; Azala-e-Auhaam Uk. 446).*

Msidhani hata mara moja kwamba Mwenyezi Mungu Atawapuuzeni; bali kwa hakika ninyi ni mbegu iliyopandwa ardhini kwa mkono wa Mungu Mwenyewe. Na Mwenyezi Mungu Yuwatangaza akisema, mbegu hii itachipuka na kukua na kutoa matawi yake kila upande na kuwa mti mkubwa mno.

Basi, amebarikiwa yule alitumainiaye neno la Mungu wala asiyaogope majaribio ya muda. Kumbukeni kwamba ni sharti majaribio yaje ili kwamba, kwa njia hii Mwenyezi Mungu Apambanue ni yupi mionganii mwenu aliye mwaminifu katika maagano yake ya baiati na ni yupi arudiye nyuma kwa visigino vyake. Atelezaye katika majaribio hatamdhuru Mwenyezi Mungu kwa vyo vyote vile nayo bahati yake mbovu mwishowe itamfikisha motoni. Laiti asingalizaliwa. Ama kwa wale watakaostahimili hadi mwisho, licha ya kukabiliwa na mikasa

mingi na kupita kwenye vipindi vyatutishaa na misukosuko; wale wenye kuzomewa na kuchekwa na mataifa, na ambaao ulimwengu utawatazama kwa dharau kubwa, ndio hatimaye watakaokuwa washindi, na milango ya baraka itafunguliwa wazi kuwakaribisha.

Na Mwenyezi Mungu Ameniamuru Alipoongea nami ya kwamba nibainishe kwa wafuasi wangu kwamba hao mionganini mwa watu walioniamini na imani yao haina shabaha za kidunia wala haina dosari ya woga na unafiki, hiyo yao ndiyo imani isiyoweza kuhalifu kanuni za utiifu katika daraja yo yote. Hao ndio wapenzi wa Mwenyezi Mungu. Ni kuwahusu wao Mungu Anapotangaza kwamba wanakanyaga njia ya ukweli.

(*Roohani Khazain Jal. 20, Uk. 309: Al- Wasiyyat Uk. 11*).

Basi sikilizeni enyi mnajihesabu kuwa wa Jumuiya yangu, mtakapokanya kikweli njia ya utawa, hapo ndipo mtakapohesabiwa mbinguni kuwa wa Jumuiya yangu. Hivyo basi, simamisheni Sala tano kila siku mkihimizwa na hofu na athari ya kuwepo Mwenyezi Mungu Mweza, kana kwamba mnambwona kwa macho yenu nyinyi wenyewe. Pia timizeni ibada ya Saumu kwa uaminifu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, mkitimiza sawasawa nguzo zote za Saumu. Kila mmoja wenu anayewajibika kutoa Zaka, naatoe. Halikadhalika, ye yote mionganini mwenu ambaye kuhiji ni faradhi juu yake wala hapana udhuru wo wote halali wa kutohiji, basi ni sharti atimize ibada ya Haji. Fanyeni wema kwa njia bora na acheni maovu kwa kuyachukia. Kumbukeni ya kwamba hapana tendo lenu lenye utovu wa utawa litakalokubaliwa na Mwenyezi Mungu. Tendo la wema ni lile ambalo mzizi wake ni kumwogopa Mwenyezi Mungu. Tendo lililo na mzizi huu, halitaruhusiwa kupotea bure. Hapana budi kwamba nyinyi mtajaribiwa kwa majaribio ya aina aina ya maumivu na hasara, jinsi walivyojaribiwa waaminio wa kabla yenu. Kwa hivyo, daima jihadharini ili msije mkateleza. Ardhi haiwezi kuwadburuni kwa vyo vyote, ikiwa mmefungamana na mbingu.

Msiue haki kwa kushiriki dhuluma. Ikubalini haki japo kama iwafikieni kwa kinywa cha mtoto. Halikadhalika, mgunduapo adui yenu kuwa mwenye haki, basi acheni mara moja upinzani wenu mkavu. Shikamaneni na ukweli na toeni ushahidi wa haki. Kumbukeni jinsi Mola Mwenye adhma Anvyowanasihini Akisema:

## فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْأَوْثَانِ وَاجْتَنِبُوا قَوْلَ الزُّورِ

Hii ina maana ya kwamba jiepusheni na chukizo la masanamu na jiepusheni na kusema uwongo ambao sio dhambi hafifu kuliko ibada za masanamu. Cho chote kinachokubetua kandoni mwa shabaha yako halisi, basi hicho ni sanamu katika njia yako. Toeni ushahidi wa kweli japo iwe dhidi ya baba zenu au kaka zenu au marafiki wenu. Wala uadui wa watu usiwachochéeni kuamua cho chote minghairi ya haki.

Msifanyiane uchoyo, msionyeshe chuki, msiwe na vivu na nyoyo zenu zisikose ukunjufu. Mafundisho ya Kurani Tukufu yaweza kugawanywa sehemu mbili kubwa. Ya kwanza ikiwa Umoja wa Mungu, na mapenzi na utiifu Kwake, Yeye Ambaye Jina lake litukuzwe. Ya pili ni kuwatendea kwa huruma nduguzo na wanadamu wenzako.

(*Roohani Khazain fal. 3 Uk. 550; Izala-e-Auham sehemu ya pili Uk. 450*).

Shikamaneni na ukweli na kuuzingatia daima. Yeye (Allah) Huona yaliyomo miyoni mwenu. Je, mtu aweza kumdanganya? Je, ujanja waweza ukawa na manufaa yo yote dhidi Yake?

(*Roohani Khazain jal. 3 Uk. 549; Izala-e-Auham sehemu ya pili Uk. 449*).

Mkitaka Mwenyezi Mungu Awe radhi juu yenu huko mbinguni, basi unganeni kama ndugu wawili waliozaliwa toka tumbo moja. Mbora wenu ni yule mwenye kusamehe sana makosa ya nduguze, na mwenye bahati mbaya ni yule mshupavu asiyesamehe, basi huyu hana fungamano nami.

Siku zote ogopeni laana ya Mungu, kwani Yeye ni Mtukufu tena Mwenye ghera. Mwovu hawezi kupata ukaribu kwa Mungu. Mwenye kiburi hawezi kumkaribia. Mdhalimu hawezi kumkaribia. Haini hawezi kumkaribia. Na kila asiye na ghera kwa jina Lake hawezi kumkaribia. Na wale wanaoangukia dunia kama mbwa na sisimizi na mbesi na wanafurahia dunia hawawezi kumkaribia. Kila jicho bayá liko mbali

naye na kila moyo mchafu hauna habari naye. Atakayekuwa katika moto kwa ajili ya Mungu, ataokolewa katika moto. Mwenye kulia kwa sababu ya Mungu atakuja cheka. Na mwenye kujitenga mbali na dunia, atakutana naye. Kuweni wapenzi wa Mungu kwa ukweli wa mioyo yenu na kwa shauku sana na kwa hamu nyingi ili Mungu pia Awe Mpenzi wenu. Rehemuni walio chini yenu na wake zenu na walio maskini katika ndugu zenu, nanyi mtarehemwiwa mbinguni vile vile. Kuweni wa Mungu ki-kweli kweli naye Atakuwa wa kwenu.

(*Roohani Khazain Jal. 19, Uk. 14-15: Safina ya Nuhu Uk.9*).

Nainasihi Jumuiya yangu kuepukana na kiburi kwani kiburi chamchukiza mno Mungu Bwana wa fahari. Pengine hamfahamu vyema kiburi ni nini? Hivyo kieleweni toka kwangu kwani mimi naongea kwa roho wa Mungu.

Kila amdharauye nduguye kwa sababu anajiona kuwa ameelimika zaidi, au mwenye maarifa zaidi, au amestawi zaidi kumshinda, basi huyo ni mwenye kiburi. Ni mwenye kiburi kwa sababu badala ya kumfanya Mungu kuwa ndiye chemchem ya elimu zote na maarifa, ye ye anajitukuza. Je, Mungu Hawezi kumpindua akili na badala yake kumjaalia elimu ya juu zaidi, maarifa na uhoodari yule nduguye amfikiriaye kuwa duni? Halikadhalika, ana kiburi yule ambaye, katika kuthamini utajiri wake au cheo chake kikubwa, anamdhara nduguye. Ana kiburi kwa sababu ya kutojali ukweli kwamba cheo chake na hadhi amevipewa na Mungu. Ni kipofu wala hafahamu kwamba Mungu Anao uwezo wa kumshushia misiba kiasi hiki kwamba ghafla adhalilike kupindukia; na kisha Anao uwezo wa kujaalia utajiri mkubwa na ufanisi juu ya yule ndugu yake anayemfikiria kuwa dhalili. Isitoshe, ni mwenye kiburi yule mtu anayejigambia ubora wa afya yake au uzuri wake, au sura yake nzuri au nguvu zake au uwezo wake, na kwa dharau humkejeli nduguye na kumkera na kumwita kwa majina ya dharau; na bila kutosheka na haya anatangaza udhaifu wa nduguye. Anakuwa na kiburi kwa sababu hatambui kuwepo kwa Mungu Ambaye Anao uwezo wa kumpiga kwa ghafla kipigo cha ulemavu wa maungo ambacho kingelimpanya dhaifu kuliko nduguye.

(*Ruuhani Khazain Jal. 18, Uk. 402: Nuzul-ul-Masih U. 26*).

## KUWASINGIZIA WENGINE

Kusingizia na kunasibisha dhana mbaya juu ya matendo ya watu wengine ni maradhi na dhamira mbovu nafsini mwa mtu inayochafua uzuri wa imani yake na utawa na huiunguza kwa haraka kama vile moto uunguzavyo majani makavu. Zama wauguao maradhi hayo wawafanyapo Manabii shabaha za mashambulio yao na kuwasingizia, Mungu huwa adui wao Naye Huwalinda Manabii Wake. Hulinda heshima ya wapenzi Wake kwa ghera isiyo na kifani. Nilipozozwa na kushambuliwa kwa njia mbali mbali, ghera hiyo hiyo ya Mungu ikawa ngao ikajitokeza kunilinda.

(*Roohani Khazain Jal. 20: Al-Wasiyyat Uk. 26 maelezo*).

Nawaambieni kwa kweli ya kwamba tabia ya kuwasingizia wengine ni maradhi mabaya yachafuayo imani ya mtu, humtoa mtu ukwelini na kuwageuza marafiki wote wakawa maadui. Ili kuzifikia sifa za daraja tukufu ya Usidiki (*Siddeeq ni lakabu inayotumiwa na Kurani Tukufu kwa ajili ya wale wenye daraja ya juu ya kiroho chini ya daraja ya Unabii*) mtu hana budi kutupilia mbali tabia mbaya ya kuwasingizia wengine. Endapo kwa bahati mbaya na bila kukusudia mtu anawasingizia wengine, basi ni sharti atubu mara moja na kuomba msamaha mfululizo na kumwomba Mwenyezi Mungu kwamba alindwe asirudie kosa hili tena na aepushiwe matokeo yake.

(*Malfoozat Jal. 11, Uk. 356*).

Ni vyema kwenu nyinyi kuwahurumia wengine na kujitakasa ili kwamba kwa kufanya hivyo muweze kupata kwa kiasi fulani sifa za Roho Mtakatifu. Kumbukeni ya kwamba bila Roho Mtakatifu utawa halisi hauwezi kupatikana. Achilieni mbali tamaa ya kinyama, na kanyageni njia ifikishayo kwenye radhi ya Mwenyezi Mungu, japo kama iwe finyu na ngumu kiasi gani. Msijitumbukize ndani ya raha za dunia, kwani huwasukumeni mbali na Mwenyezi Mungu. Ni afadhali machungu yampendezayo Mungu kuliko raha inayomchukiza. Kule kushindwa kumpendezako Mwenyezi Mungu ni bora kuliko ushindi umchukizao. Jiepusheni na matamanio yawabururayo moja kwa moja kwenye

ghadhabu za Mwenyezi Mungu. Mkimjia kwa moyo, Yeye Atawasaidieni kwa kila njia wala hapana adui atakayeweza kuwadhusuni.  
*(Roohani Khazain Jal. 20 Uk. 307: Al - Wasiyyat Uk. 9).*

“Vazi la utawa” ni msemo wa Kurani Tukufu. Hii inaashiria kwenye ukweli kwamba uzuri na mapambo ya kiroho vyaweza kupatikana tu kwa njia ya utawa. Na hakika ya utawa ni kwamba mtu kwa uwezo wake wote, atimizie wajibu wake kuhusu vipawa vyake na ahadi ya imani ya Mungu kama amana. Pia ni sharti atilie maanani wajibu wake kwa wanadamu wenzake na viumbe vyote vya Mungu kama amana aliyokabidhiwa. Yaani akanyage njia ya utawa kikamilifu sawa na uwezo wake wote.

*(Roohani Khazain Jal. 21, Uk. 210: Braheen-e-Ahmadiyya sehemu V Uk. 210).*

Mungu Yule (Awasilishwaye na Kurani Tukufu) ni Mungu Mwaminifu kabisa kabisa, Atimizaye maajabu kwa ajili ya wale wadumuo kumwamini. Ulimwengu wadhamiria kuwaangamiza (wamwaminio Mwenyezi Mungu), lakini Yeye Anayesuhubiana nao Huwaokoa toka kila janga na kuwapatia ushindi katika kila uwanja. Ni mwenye bahati kubwa kiasi gani yeye adumishaye fungamano lake na Mwenyezi Mungu.

*(Roohani Khazain Jal. 19, Uk. 20: Safina ya Nuhu).*

## WAHYI

Mwenyezi Mungu anapotaka kumfahamisha mtumishi Wake jambo la ghaibu, iwe afanya hivyo katika kujibu maombi ya mtumishi Wake au kwa kudra Yake, humletea aina fulani ya mzimio na ghafla huyatoka mazingara yake. Katika hali hiyo, fahamu zake huzimika kiasi cha kujisahau hata yeye mwenyewe. Kama mpiga mbizi kwenye kina cha bwawa, yeye hufunikizwa kabisa na kuzama ndani ya ile hali ya kutojifahamu, kutojitambua na kuzimia. Mwishowe anapozinduka na hali ya mzimio kuondolewa, anakumbuka sauti nafsini mwake. Sauti ile inapotoweka anatambua kuwemo nafsini mwake maneno matamu, fasaha na adhimu bila kifani. Na uzoefu huu ni wa ajabu wenyewe adhma kiasi hiki kwamba mtu hawezi kuuelezea kwa kauli ya mdomo. Ni uzoefu huu umfunuliao mtu kuwepo kwa mtiririko wa mto wa elimu ya ndani. Ni kwa njia ya uzoefu huu unaokaribiana sana na kuzirai ambapo mtumishi wa Mungu anapokea toka kwa Mwenyezi Mungu majibu ya maombi yake yote kwa sauti tamu mno iliyo fasaha. Na katika kujibu swali lolote linalozuka katika hali inayofanana na kuzirai, Mwenyezi Mungu Humfunulia elimu ya ndani sana mtu asiyoweza kuvumbua kwa njia nyinginezo zote. Uzoefu huu wenyewe huimarisha imani ya mtu juu ya Mwenyezi Mungu na kumwezesha kuzielewa vyema zaidi kanuni Zake za ajabu. Maombi ya mwanadamu na majibu yake toka kwa Mwenyezi Mungu kwa njia ya kudhihirisha kwamba Yeye Ndiye shabaha halisi ya ibada ni jambo limwezeshalo mwanadamu kumtazamia Mwenyezi Mungu kana kwamba anamwona hapa hapa duniani; hivyo basi yeye huanza kuwa wa dunia zote mbili kwa sambamba.

(*Roohani Khazain Jal. 1, Uk. 260-62 maelezo; Braheen-e-Ahmadiyya*).

Katika aina nyingine ya wahyi usiohusikana kamwe na uzoefu wa matamanio ya moyoni, mtu husikia sauti ya nje kana kwamba yupo mwongeaji anayeongea nyuma ya pazia. Sauti hii ni tamu mno na changamfu na matamshi yake huelekea kuwa ya haraka haraka yakiujaza moyo wa mtu. Pengine hutokeea kwamba akili ya mtu imejaa mawazo mengi na ghafla sauti hii husikika. Baada ya kusikia sauti hii yeye huachwa akistaajabia ilikotoka na nani yule aliyeongea naye. Kisha hutazama huku na huku kama mtu aliyeshangaa, na hapo kuanza kutambua kwamba sauti ile ilitoka kwa Malaika. Mara nyingi sauti hii toka nje husikika ikiwemo habari njema zama mtu anapokuwa

ametumbukia katika hali ya hofu kubwa na huzuni kuhusu matatizo fulani.

(*Roohani Khazain Jal. 1, Uk. 287, Maelezo: Braheen-e-Ahmadiyya*).

Imekwisha faridhiwa kwamba mtu mwenye nuru kiasi fulani ataongezwa nuru. Na asiyekuwa na cho chote hapewi cho chote. Mtu aliyejaaliwa kipawa cha kuona ndiye anayefaidika kutokana na mwangaza wa jua. Vivyo hivyo mtu asiyekuwa na macho huendelea kutoweza kuona mwangaza wa jua. Ni kweli kabisa ya kwamba mwenye nuru haba ndani ya nafsi yake, pia hupata nuru haba toka nje ya nafsi yake. Yule aliyejaaliwa kwa wingi zaidi nuru ya ndani ya nafsi yake vile vile atafaidika kwa wingi zaidi kutokana na nuru ya nje. (*Roohani Khazain Jal. 1, Maelezo uk. 195-96: Braheen-e-Ahmadiyya*)

Mwenyezi Mungu ameyagawanya malimwengu (Universe) Yake ya ajabu katika mafungu matatu. Kwanza, ulimwengu wa dhahiri unaoweza kufahamika kwa njia ya macho na masikio na viungo vingine vya hisia, moja kwa moja au kwa msaada wa ala.

Pili, ulimwengu wa ghaibu unaoweza kufahamika kwa kutumia busara njema na mifano.

Tatu, ulimwengu ulioko mbali zaidi ya ule wa ghaibu, mgumu kufahamika hata waelekea kutofikika kimawazo. Ni wachache sana wafahamu kuwepo kwake. Huo ni ulimwengu ulio siri kubwa usioweza kufahamika vyo vyote ila kuwazia tu. Ni kwa njia ya jicho la kiroho tu au wahyi au uzungumzi wa Mwenyezi Mungu, mtu anaweza akaufikia ulimwengu huo wala si kwa njia nyingineyo iwayo. Kama ionekanavyo katika kudra ya Mungu idhihirikayo katika maumbile, mtu asingekosea afikiapo uamuzi ya kwamba kama vile ambavyo Mwenyezi Mungu amemjaalia mwanadamu ala na vifaa vya kufahamia aina mbili za kwanza za uumbaji Wake zilizotajwa hapo juu, vivyo hivyo ni sharti awe amemjaalia mwanadamu ala na vifaa vya kuufahamia ule ulimwengu wa uumbaji Wake wa aina ya tatu. Na ala zenyewe (kama tulivyosema juu) ni pamoja na jicho la kiroho, wahyi na maneno ya Mwenyezi Mungu. Mawasiliano sampuli hii hayawezi yakasemwa kwamba eti hayapo au kwamba yamepata kukatizwa katika zama zo zote zile. Siyo, bali wale waliohitimisha masharti yake wamefunguliwa mlango wa mawasiliano haya na watandelea kujaaliwa vivyo hivyo. (*Roohani Khazain Jal. 2: Surma Chashm-e-Arya Uk. 127 Maelezo*)

## MALAIKA

Mtu hugundua kutokana na tafakuri ya ndani ya Kurani Tukufu ya kwamba sio kwa ajili ya elimu na ulezi wa wanadamu tu, bali pia kwa ajili ya maendeleo ya nje na ndani ya malimwengu yote, ni lazima wawepo watumishi baina ya Mungu na viumbe vyake. Vipo vidokezo bayana katika Kurani Tukufu vinavyomfanya mtu kuamini kwamba viumbe watakatifu waitwao Malaika wanao uhusiano na sayari mbali mbali za mbinguni. Baadhi yao kwa vipawa vyao maalumu, wanazisimamia nyendo za pepo, na wengine hufanya mvua inyeshe. Halikadhalika, wapo wengine waliokabidhiwa jukumu la kusababisha athari zingine za kimbunguni zishuke ardhini.

(*Roohani Khazain Jal. Uk. 70: Tauzeeh-e-Maram Uk 22*).

Ifahamike kwamba sawa na Islam, kimaumbile Malaika hawana vipawa bora kuliko vile walivyo navyo wanadamu. Jambo la kupewa kwao utumishi katika ulimwengu wa dhahiri au ule wa kiroho lenyewe sio alama ya kuonyesha ubora wao. Sawa na mafundisho ya Kurani Tukufu wao hupewa majukumu haya kama watumishi.

(*Roohani Khazain Jal. 3, Uk. 74: Tauzeeh-e-Maram, Uk. 26*).

Basi kushuka kwa Malaika maana yake ni nini? Mtu aweza akashangaa. Hivyo ifahamike ya kwamba sawa na kanuni za azali za Mwenyezi Mungu, Mjumbe au Nabii au Muhaddith ashukapo toka mbinguni kuja kuwarekebisha wanadamu, daima hushuka pamoja naye Malaika wenye kazi ya kupanda mbegu ya mwongozo katika miyo mielekevu. Huifanya ilekee kwenye wema. Huendelea kushuka vivyo hivyo mpaka pale giza la ujinga, na ujisadi linapokucha kwa mwangaza wa siku mpya ya imani na utawa.

Kurani yaelezea ukweli huu katika aya isemayo:

تَنْزَلُ الْمَلِكَةُ وَالرُّوحُ فِيهَا يَادُنِ رَبِّهِمْ مِّنْ كُلِّ أَمْرٍ<sup>۱</sup>  
سَلَّمَ هِيَ حَتَّىٰ مَطْلَعِ الْفَجْرِ<sup>۲</sup>

Huteremka Malaika na Ufunuo katika huo kwa idhini ya Mola wao kwa kila jambo. Amani; na (usiku) huo (unaendelea) mpaka mapambazuko ya alfajiri (97:5-6).

Ushukaji wa Malaika na Roho Mtakatifu hutokea zama ashukapo ardhini mtu mwenye sifa tukufu na mwenye vazi la Khalifa wa Mungu na alobarikiwa kwa Neno la Mungu. Roho Mtakatifu hujaaliwa kwake kwa njia maalumu.

(*Roohani Khazain Jal. 3 maelezo, Uk. 12: Fath-e-Islam, Uk. 12*).

## KUJITAHIDI KATIKA NJIA YA MWENYEZI MUNGU

Islam haikupendekeza karaha. Kurani Tukufu na vitabu vyat Hadithi kama vichunguzwe kwa uangalifu, na visomwe na kusikizwa kwa makini kadri inavyowezekana, mtu hana budi kufikia thabiti ya kwamba yale masingizio eti Islam iliruhusu utumizi wa upanga ili kuzagaza dini ni masingizio ya aibu yasiyo na msingi wowote. Kusema kweli, hizi ni dhana za wale tu ambao hawakupata kusoma kwa nia njema Kuruani Tukufu au Hadithi au historia sahihi ya Kiislamu. Si hayo tu, bali baadhi yao bila kuona haya wametunga uwongo na uzushi. Na juu ya kwamba wakati unakaribia upesi sana ambapo wale wote wenye njaa na shauku ya kutaka ukweli watatambua udanganyifu wa jamaa hao. Yawezaje dini kuitwa dini ya mabavu ambayo kitabu kitakatifu chapiga marufuku utumizi wa mabavu kwa shabaha ya kuzagaza imani? Ndiposa Kurani Tukufu ikatangaza ikisema:

لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ قُلْ

Yaani: “Hakuna karaha katika dini” (2:257).

Je, twaweza kumshutumu yule Nabii Mtukufu kwamba alitumia mabavu dhidi ya watu wengine, ambaye, kwa muda wa miaka kumi na mitatu, usiku na mchana, aliwashauri Masahaba wake kutolipa ubaya kwa ubaya, bali wavumilie na kusamehe? Hata hivyo, zama ukorofi wa maadui ulipofurika, na ule wakati watu wote pembezoni mwake walipofanya kila juhudili ili kuangamiza Islam, ile sifa ya Mwenyezi Mungu kwamba Yeye daima Huwalinda wapenzi Wake ikaamrisha ikisema:

“Acha wale walioshika upanga waangamie kwa upanga”

Waila, Kurani Tukufu haikuruhusu karaha katika dini kwa njia yo yote iwayo. Kama ingelikuwa imetumika karaha kwa njia yo yote katika Kujichumia wafuasi na Masahaba wa Mtume Mtukufu s.a.w. wangelikuwa matunda ya karaha, isingeliwezekana kwao wakati wa

dhiki kuonyesha subira na uaminifu mkubwa ambao ni waaminio wa kweli tu peke yao wawezao kuonyesha. Utiifu na uaminifu wa Masahaba wa Bwana wetu, Mtume Mtukufu (S.A.W.) ni jambo lijulikanalo sana kiasi hiki kwamba halihitaji maelezo zaidi toka kwetu sisi. Ni wazi kabisa kwamba mionganii mwao imo mifano ya utiifu na subira ilio vigumu kuupata mfano wake katika historia za mataifa mengine. Kundi hili la waaminio halikutikisika katika utiifu na subira yao hata wakichomolewa panga. Kinyume chake walipoandamana na Nabii wao Mkuu na Mtakatifu, amani na baraka za Mungu ziwe juu yake, wao wakaonyesha subira ambayo hapana mtu awezaye kuonyesha ila moyo wake na kifua chake viwe vimeangaziwa nuru ya imani. Ndipo sasa karaha haikuwa na wajibu wo wote wa kutimiza katika Islam.

*(Roohani khazain Jal. 15: Masih Hindustan Mein Utangulizi, Uk. 11-12)*

Hapana hata mmoja wa Waislamu wanyofu waliopata kuishi duniani aliyekuwa na imani kwamba yafaa itumike karaha katika kuzagaza Islam. Kwa upande mwingine, Islam daima imestawi kwa nguvu ya sifa zake za azali za ubora. Ama kwa hakika hawaelewi uzuri wa asili wa Islam wale ambao pamoja na kubahatika kuitwa Waislamu wanaelekea kuamini kwamba yafaa Islam kuenezwa kwa mabavu.

*(Roohani Khazain Jal. 15: Tiryaq-ul-Qulub, Uk. 35, Maelezo).*

## **MAOMBI**

Zama zinapokuwa karibu baraka za Allah, Yeye Hutimiza masharti yote ya kukubaliwa maombi. Moyo hutiwa duku-duku, hupata joto na kuanza kung'aa. Lakini, kama sio wakati wa maombi kukubalika, basi moyo hukosa ile hali iufanyao kuelekea kwa Mwenyezi Mungu. Hata kama mtu ajitutumue kiasi gani, moyo hukataa kuonyesha uelekevu. Hivi ni kwa sababu nyakati zingine Mwenyezi Mungu Hushikilia hukumu Yake ili Amri Yake itimie na nyakati zingine huziridhia dua za mtumishi Wake.

Hii ndiyo sababu nikosapo kuhisi alama za kibali cha Mwenyezi Mungu, mimi sipati tumaini la kupokelewa maombi. Katika wakati kama huo mimi husalimu Amri ya Mola wangu kwa furaha kubwa zaidi ya ile nipatayo kwa kukubaliwa maombi. Najua bila shaka, kwamba baraka na matunda ya kusalimu Amri ya Mwenyezi Mungu ndiyo mengi zaidi.  
*(Malfoozat Jal. 1, Uk. 440)*

## IMANI ZETU

Muhtasari wa imani yetu ni:

*La Ilaha Illallah Muhammadur Rasulullah.* Yaani hapana Mungu ila Allah na Muhammad ni Mtume Wake. Imani yetu, tunayoizingatia katika maisha haya ya humu duniani na ambayo tutadumu kuishikilia mpaka tutakapoingia Akhera, ndiyo hii kwamba Kiongozi wetu wa kiroho na Bwana wetu, Muhammad, amani na baraka za Mungu ziwe juu yake, ndiye Muhuri wa Manabii na Mbora wa Mitume wote. Kwa mikono yake dini imekamilika, na imetimizwa ile baraka imwongozayo mwanadamu kwenye njia ya haki na mbele zaidi hadi kufikia kwa Mungu Mwenyewe. Sisi twaishikilia imani hii halisi kwa yakini kabisa ya kwamba Kurani Tukufu ndiyo muhuri wa vitabu vyote vya Mungu, wala hapana mazidisho yo yote au mapunguzo yo yote yawezayo kufanywa katika mafundisho yake, makatazo, maamrisho au maagizo yake. Hautakuwepo wahyi au neno la Mungu litakaloweza kusahihisha au kufuta au kubadilisha au kugeuza mafundisho ya Kurani Tukufu. Sawa na maoni yetu, hawi mionganoni mwa kundi la waaminio bali yu kafiri yule mwenye kutazamia ujaji wa kitabu kitakachotangua Kurani Tukufu.

(*Roohani Khazain Jal. 3: Izala-e-Auham*).

(Kidokezo) (Haya yamo ndani ya Tambio ya Mubahala).

Enyi mkaao ardhini! Na enyi roho za watu wakaao mashariki au magharibi! Nawakaribisheni mkubali ukweli kwamba leo hii, dini pekee ya kweli humu duniani ni Islam na Mungu wa kweli ni Yule Mungu Ambaye Ametajwa ndani ya Kurani Tukufu, na yule Nabii mwenye uzima wa kiroho wa milele - yule akaliaye kiti cha fahari na utawa - ni Mtume Mtukufu Muhammad, Mteule, S.A.W.

(*Roohani Khazain Jal. 15: Tiryaq-ut-Qulub Uk. 7*).

## DHAMBI

Dhambi - ambayo kusema kweli ni sumu - hupatikana pale mtu akosapo utiifu kwa Mwenyezi Mungu na anapokuwa na utovu wa upendo Wake na kumbukumbu Yake yenye shauku. Hakika ya mtu ambaye moyo wake umeganda dhidi ya mapenzi ya Mungu ni sawa na mti uliong'olewa na hauwezi tena kunyonya lishe ya uzima toka ardhini. Katika hali kama hiyo pole pole mti hunyauka na kufa, hivyo chambiliche kukauka kwa mti, dhambi huusibu moyo. Tiba za ukavu huu, sawa na kanuni za maumbile, ni za aina tatu.

(1) Upendo, (2) Istighfar, yaani kumwomba Allah msamaha. Kiuzungumzi, hii ina maana ya kutamani kuzika au kufunika, ikimkumbusha mtu ya kwamba mradi mzizi wa mti umezikika ardhini lipo tumaini la mti kuota tena majani mapya. (3) Tiba ya tatu ndiyo tauba (toba) hii ikiwa na maana ya kumgeukia Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu kujivutia lishe ya uzima, na mtu kujisogezza karibu naye zaidi, na kujichubua kwa msaada wa matendo mema gamba la madhambi alilo nalo. Toba haipatikani kwa maneno matupu ya mdomo; kusema kweli, toba yaweza tu kukamilika kwa msaada wa matendo ya kitawa. Matendo yote ya wema yana lengo la kufikia ukamilifu wa toba.

*(Roohani Khazain Jal. 12, UK. 328: Sirajuddin Isai ke char Sawalon ka Jawab Uk. 2-3)*

## **WOKOVU**

Itikadi ya wokovu (kwamba ukombozi waweza ukapatikana kwa kumtundika Yesu (a.s.) isemwavyo katika Injili, yakataliwa na Kurani Tukufu. Licha ya ukweli kwamba Kurani Tukufu yamthibitisha Yesu kuwa Nabii mheshimiwa wa Mwenyezi Mungu, na kumtangaza kwamba yu mpPENDWA na karibu wa Mwenyezi Mungu, na yamwelezea kuwa wa umbo adhimu la kuheshimika, lakini hata hivyo yambainisha kwamba alikuwa mwanadamu. Pia Kurani Tukufu yaikatalia mbali kimsingi dhana kwamba kwa minajili ya ukombozi, mzigo wa mwenye dhambi unaweza ukahamishwa kwa mtu mwingine asiye na dhambi. Vivyo hivyo mizani ya akili ya mwanadamu haikubali wazo kwamba mtu mmoja, Dicki, aadhibiwe kwa ajili ya dhambi za mtu mwingine, Tomaso. Hata serikali za kidunia hazifuati kawaida kama hii. Lahaula, kumbe Maarya (dhehebu la Baniani) nao wamefanya kosa walilolifanya Wakristo juu ya dhana ya ukombozi. Hawa pia wamekosea. Sawa na itikadi za Kiarya, toba na kuomba msamaha ni mambo yasiyo na faida. Kuzalika-zalika (*reincarnation*) kwa roho ikiwa ndiyo adhabu itolewayo na itikadi za Kiarya, wao wanaamini kwamba isipokuwa roho ya mtu izalike-zalike mara nyingi hata awe ametenda dhambi moja tu, wokovu hauwezi ukapatikana kwa ajili yake.

(*Roohani Khazain Jal. 23, Uk. 414: Chashma-e-Marifat Uk. 44*)

## **MAISHA BAADA YA KIFO**

Islam yatoa mafundisho bora kabisa ya kwamba mara baada ya kifo, kila roho hupata namna fulani ya mwili mpya amba ni wa lazima kwa ajili ya kuonjea raha ama adhabu. Hatuwezi kusema kinaga-ubaga mwili wenyewe huumbwa toka vitu gani. Kadri mwili huu wa udongo unavyohusika, kuwepo kwake hukoma baada ya kifo. Aidha, haijapata kudaiwa na ye yote kwamba mwili huu wa udongo hufufuliwa kaburini. Kinyume chake, mwili huu mara nyingi huchomwa moto, na kuna nyakati ambapo mwili huu huhifadhiwa katika majumba ya kuwekea sanaa, au kuwekwa kwa njia nyingine nje ya kaburi kwa muda mrefu. Kama ingelikuwa mwili huu wa udongo ndio unaofufuliwa, yaelekea sana kwamba watu wangekuwa tayari wamekwisha lishuhudia jambo hili likitendeka. Hata hivyo, kufufuliwa kwa wafu kwabainika sana mtu asomapo Kurani Tukufu. Ndipo sasa mtu analazimika kuamini kwamba wafu hufufuliwa wakiwa katika hali tusiyoweza kuiona. Upo uwezekano kwamba ule mwili wa kiroho hutokana na vitu vilivyochujwa sana vya mwili huu wa udongo. Roho ikisha vishwa mwili huo mpya, sasa hurejeshewa tena hisia zake za kibinadamu. Kwa kuwa mwili huu mpya huwa mwepesi mno na wa kimbunguni katika khulka, mandhari iliyo pana zaidi ya busara na ufunuo hufunguliwa kwake.

*(Roohani Khazain Jal. 13, Uk. 70-71: Kitab-ul-Bariya Uk. 52)*

## ROHO

Uchunguzi waonyesha kwamba mwili ndio mama wa roho. Roho haimdondokei mama mja mzito toka juu mawinguni. Badala yake roho ni aina ya nuru iliyomo ndani ya mbegu ya uzazi ambayo huanza kung'aa kufuatana na ukuaji wa mtoto tumboni. Wahyi mtakatifu wa Mungu watuwezesha kufahamu kwamba roho huchujwa kutoka chimbuko la mimba liumbikalo ndani ya tumbo la uzazi kutokana na mbegu ya uzazi. Kama Mwenyezi Mungu asemavyo katika Kurani Tukufu:

ثُمَّ أَنْشَأَنَّهُ خَلْقًا أَخْرَمْ فَتَبَرَّكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَلِيقَينَ ﴿٦﴾

Yaani, kisha katika ule mwili ulioumbika katika tumbo la uzazi, Twadhihirisha kiumbe kingine kiitwacho roho. Na ni Mwenye Mibaraka Mungu Aliye Mbora wa waumbao (23:15). Na kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Chemchem ya baraka nyingi na ni Mwumbaji Asiyekuwa na mfano wake.

*(Roohani Khazain Jal. 10: Hekima ya Mafundisho ya Kiislamu Uk. 7)*

Kama isivyowezekana kwa bustani yo yote kustawi bila ya maji, vivyo hivyo hapana imani iwezekanayo kufikiriwa kuwa hai bila ya matendo mema. Haina maana kuwa na imani bila matendo ya kitawa; hali kadhalika, matendo mema bila ya imani ni upuuzi mtupu. Sawa na mafundisho ya Islam, hakika ya pepo ni onyesho la picha ya imani na matendo yetu mema. Wala sio kitu kipyta atakacholetewa mtu toka nje, kusema kweli pepo huumbwa kutoka ndani ya nafsi ya mtu. Pepo ya kila mtu huzalika kutokana na imani na matendo yake mema, ambayo yeye huanza kupata uzoefu wake na kuifurahia katika maisha haya haya.

*(Roohani Khazain Jal. 10: Hekima ya mafundisho ya Kiislamu Uk. 85)*

## **HAKIKA YA YAJUJA NA MAJUJA**

Yajuja na Majuja ni watu wawapitao wengine wote katika utaalamu wao wa matumizi mbali mbali ya moto na ambao kwa kweli ndio wavumbuzi katika uwanja huu. Majina yao yenyewe (Tambua: katika lugha ya Kiarabu maneno Yajuj na Majuj yanatokana neno *ajuj* lenye maana ya moto) yanadokezea kwamba uvumbuzi wao wote, iwe ni merikebu, gari moshi au mashine zingine, vingeliendeshwa kwa nishati ya moto. Nao wangepigana vita vyao kwa silaha za moto. Wangeyapita mataifa yote mengine ardhini katika uwemo wa kuufanya moto uwahudumie. Ndio maana, wao wanaitwa Yajuja na Majuja. Hivyo, bila shaka hayo ni mataifa ya Ulaya ambao katika sayansi ya matumizi ya moto, wao ni stadi kupindukia, ni mafundi werevu na mashuhuri kiasi hiki kwamba haina haja kuelezea zaidi. Ni watu hao hao wa Ulaya walioitwa Gogu na Magogu katika vitabu vya kale walivyopewa Manabii wa Kiisraeli. Mji wa Moscow uliokuwa makao makuu ya Urusi (Roshi) umetajwa kwa jina. Ilikadiriwa kwamba Masihi Aliyahidiwa angedhiihiri katika zama za Yajuja na Majuja.

*(Roohani Khazain Jal. 14: Ayyamus Sulh Uk. 182-83).*

## MSIMU WA MWANGAZA

Kama mnavyofahamu matunda huja kwa msimu wake, hivyo hata Nuru nayo pia hushuka kwa msimu wake; na hapana awezaye kuifanya ishuke kabla haijaja yenyewe, wala mtu hawezo kuizuilia njia yake zama ianzapo kushuka. Utakuwepo ugomvi na ubishi, lakini hatimaye Ukweli utapata ushindi. Sababu yenyewe ni kwamba hii sio kazi ya mwanadamu. Hii ni kazi ya Mwenyezi Mungu Abadilishaye misimu, Hugeuza nyakati, na Huutoa mchana toka usiku na usiku toka mchana. Ingawa Yeye Huumba giza pia, lakini Anachotaka hasa ni mwangaza. Yeye pia Huiacha izagae ibada ya masanamu, lakini Yeye kwa kweli, Anachotaka kuona kikistawi ni Umoja (wa Mungu). Haridhii kwamba adhma Yake wawe nayo wengine. Tangu kuumbwa mwanadamu hadi wakati ule atakapofutika, hii ndiyo kanuni isiyobadilika ya kwamba daima Mwenyezi Mungu Atadumu upande wa Umoja (imanzi ya Umoja wa Mungu).

*(Roohani Khazain Jal. 15: Masih Hindustan Mein Uk. 65)*

E Mungu, E Mwumba wa vitu, Unilindaye dhidi ya aibu,  
Wewe ndiwe Hazina.

E wangu Mpandwa, wangu Mfadhili, wangu Mhifadhi.

Ni kutokana na rehema tu kwamba Umenichagua,  
Waila haukuwemo uhaba wa watumishi katika jumba Lako.

Wale waliozoea kuwa marafiki sasa wamekuwa maadui.  
Lakini Wewe hujawahi kuniacha, E Rafiki wa kweli.

E Mpandwa Usiye na mshirika, kimbilio la uhai wangu.  
Wewe wanitosha, bila Wewe mimi si kitu.

Bila huruma Zako, mimi ningelishakuwa mavumbi.  
Kisha ni vipi ama ni wapi yatupwapo mavumbi hayo,  
Ajuaye ni Allah pekee.

Natamani kiasi gani laiti katika njia Yako, uhai wangu,  
mwili wangu na moyo wangu vingetolewa sadaka.  
Sioni mwingine ye yote awezaye kupenda upendavyo Wewe.

Nimepitisha siku zangu awali chini ya kivuli cha huruma Zako.  
Ulinipakata kama mtoto anyonyaye.

Sikupata kushuhudia uaminifu mionganoni mwa wanadamu  
kama ule ulio nao Wewe.

Hayupo rafiki awezaye kuhurumia kama Wewe.

Wanasema hapana akubalikaye bila ustahilifu.  
Tazama, bila ustahilifu wo wote mimi nikapewa kao katika jumba Lako.

Umenitosa ndani ya fadhili na ukarimu,  
Kiasi kisichowenza kuhesabika hadi siku ya mwisho.

(*Roohani Khzain Jal. 21. Braheen-e-Ahmadiyya sehemu V, Uk. 127*).

## KURANI TUKUFU

Kurani Tukufu ni sanduku la johari, lakini ni wachache wanaofahamu ukweli huu. (Malfoozat Jat. 2, Uk. 344).

Kurani Tukufu ndicho kitabu chenyeh fahari kuu kiasi hiki kwamba hapana kitabu kingine kinachoweza kuipita katika fahari yake. Ndicho *Al-Hakam*, kikiwa kitabu ambacho uamuzi wake ndio wa mwisho; ndicho *Muhaiman*, yaani: Ni muhtasari mzima wa kila mwongozo. Ndani yake yapatikana kila hoja mtu awezayo kuhitaji. Ni kitabu hiki ambacho kimeitimua kwa ushindi nguvu ya maadui. Kitabu kinachozungumzia kila kitu kwa undani na kinazo habari za yale yaliyokuwepo na yale yatakayo kuwepo. Batili haiwezi kukishambulia toka mbele wala nyuma. Ndicho nuru halisi ya Mungu Mweza.

(*Roohani Khazain Jal. 16, Uk. 103: Khutba Ilhamiya Uk. 103*).

Yafaa ifahamike kwamba muujiza mkubwa zaidi wa Kurani Tukufu ni ile bahari isiyo na mipaka ya elimu yenye vina vya ndani - ukweli halisi, zile njia za Kurani Tukufu zilizojaa elimu na filosofia - tuwezazo kuzionyesha kwa uwazi mataifa yote na watu wa kila lugha: wawe Wahindi, Waajemi, Wazungu au wa Marikani, haidhuru wawe wanatoka nchi gani. Muujiza wa Kurani Tukufu unaweza ukakunjisha mikia yao, kuwanyamazisha na kuzidondosha chini silaha zao. Maana za Kurani Tukufu zaendelea kudhihirika kila itokeapo haja sawa na wakati unavyobadilika na kusimama kama askari wenye silaha nyingi dhidi ya hila na masingizio yanayozushwa katika kila zama. Lau kama Kurani Tukufu isingalikuwa timilifu kuhusu yale iliyօ nayo ya ukweli halisi na uhakika bayana, isingalihesabiwa kuwa ule muujiza mtimilifu.

Kurani Tukufu ni muujiza ambao mfano wake haujapata kuwepo wala hautapata kuwepo. Zama za baraka na neema zake ni za milele. Inaendelea kujitokeza na kung'aa wakati wo wote kama vile ilivyokuwa katika wakati wa Mtume Mtukufu wa Islam (S.A.W.) Ni lazima kutilia maanani ukweli kwamba maneno ya mtu hulingana na uthabiti wa adhma yake, ustadi na nia. Kadri kilivyo kikubwa kiasi cha ustadi wake na nia na ari yake ndivyo kitakavyo kuwa kikubwa kiasi cha ufasaha

na ubora wa maneno yake. Kanuni hii hii inatumika kuhusu wahyi toka kwa Mwenyezi Mungu. Kadri kilivyo nyanyuka kiasi cha ustadi wa mpokeaji wa wahyi, ndivyo kitakavyo nyanyuka kiasi cha mpambanuo na ubora wa wahyi wa Mungu. Kulingana na kiasi kikubwa cha adhma yake, ustadi na nia, wahyi aliofunuliwa yeye ulikuwa wa ngazi ya kileleni, ndipo sasa hawezi akazaliwa mtu ye yote atakaye kuwa sawa naye katika uwanja huu.

(*Malfoozat Jal. 3, Uk.57*).

Twasema kweli tupu wala hatuwezi kujizuia kufanya hivyo: Asingaliinuliwa Mtume Mtukufu S.A.W. na isingeliteremshwa Kurani Tukufu ambayo athari zake wakazishuhudia wazee wetu na viongozi wa Kiroho wa hapo zamani na twaendelea kuzishuhudia leo hii, ingelikuwa vigumu mno kwetu sisi, kwa msaada wa rai za Biblia peke yake kumtambua Musa na Isa na Manabii wengine wa hapo awali, kuwa mionganoni mwa lile kundi la watu wanyofu na watawa amba Mwenyezi Mungu, kutokana na rehema Zake, Aliwachagua kwamba wawe Manabii. Hatuna budi kutambua baraka hii ya kiroho ya Kurani Tukufu kwamba inadhihirisha nuru yake katika kila zama, na kisha kwa msaada wa ile nuru timilifu inatuthibitishia ukweli wa Manabii wa hapo awali. Na baraka hii hatukujaaliwa sisi peke yetu, bali walijaaliwa pia Manabii wote waliodhihiri tokea wakati wa Nabii Adamu hadi wakati wa Yesu (amani ya Mungu iwe juu yao) kabla ya kuteremshwa Kurani Tukufu.

(*Roohani Khazain Jal. 1: maelezo ya maelezo I* Uk. 290 *Braheen Ahmadiyya* Uk. 290)

Ni kosa la vipofu wenyewe, waila nuru ile, Ni angavu mno kiasi hiki kwamba hung'aa kwa mng'ao wa majua mia moja.

Ole kwa maisha ya watu kama hao hapa ardhini,  
Ambao nuru hii ilikuwa wazi kwao, lakini nyoyo zao zikaambulia kuwa vipofu.

(*Roohani Khazain Jal. 1, Braheen-e-Ahmadiyya* Uk. 304-306, *maelezo ya maelezo 2*).

Sikilizeni enyi mlo vipedzi kwangu mimi kwamba bila Kurani,  
Mwanadamu kamwe hawezu kuufikia ukweli.  
Daima huujaza moyo nuru, hutakasa kifua kabisa.  
Nawezaje kujachisha kuzitokuza sifa zake,  
Tazama! huyapatia maisha haya uhai mwengine.  
Angalia! Yang'aa mithili ya juu la utosini.

Awezaje mtu kuukana mng'ao wake.  
Kila neno lake ni bahari ya elimu,  
Humfanya mtu kunywa kikombe cha upendo wa Mungu.  
Hiyo tu ndiyo tiba ya wanaougua.  
Ishara ya pekee toka kwa Mungu ielekezayo kwa Mungu.

Hilo tu ndilo juu la mwongozo tulilolipata,  
Huyo tu ndiye mtekaji wa nyoyo tuliye patakuona.  
Lo lote wasemalo waikataao  
Hawasemi cho chote ila upuzi mtupu.

(*Roohani Khazain Jal. 1: Braheen-e-Ahmadiyya Uk. 269 maelezo ya maelezo 2*).

Miongoni mwa Vitabu vyote vilivyofunuliwa tuonavyo leo hii, ni Kurani Tukufu pekee, ambayo madai yake kwamba ni maneno ya Mungu, yanathibitishwa kwa njia ya hoja zisizosutika. Kanuni ilizotoa kuhusu wokovu zaafikiana kabisa na maelezo ya ukweli na khulka za mwanadamu. Mafundisho inayotoa ni makamilifu na yenye uhakika kiasi hiki kwamba yanaungwa mkono kikamilifu na ushahidi wenye nguvu usiopingika. Maamrishi yake hayasimami juu ya cho chote ila ukweli. Mafundisho yake yameepukana kabisa na uchafuzi wa ibada za masanamu, uzushi na kuabudu viumbi. Ni Kitabu ambacho ndani yake mna jazba kubwa mno ya kudhihirisha Umoja na Utukufu wa Mungu na kutilia mkazo ukamililifu wa sifa za Yule Mungu Mmoja tu. Ni kitabu chenyehii sifa tukufu kwamba kimejazwa kabisa tena mahsus, kwa mafundisho ya Umoja wa Mungu, hakiruhusu aina yo yote ya dosari, au upungufu, au lawama zo zote kunasibishwa na Mwumba Mtakatifu. Hakinuii kuwashurutishia watu fundisho lake

Io lote. Kinyume chake, kila kitu inachofundisha hukipatia utangulizi wa hoja na mapasiko vinavyothibitisha ukweli wake. Huthibitisha shabaha zake na makusudio kwa hoja zenyenuguu na dalili bayana. Baada ya kuwasilisha hoja wazi wazi kuelezea kila kanuni inayoiweka, kumwongoza mwanadamu hadi kufikia imani thabit na kufahamu kikamilifu mambo yalivyo. Huondolea mbali kwa njia ya miongozo safi, kasoro zote, uchafu na ubandia unaozivamia imani za watu, shughuli zao, na maneno na matendo yao. Pia yafundisha mienendo yote ilio ya lazima ili kupanda mbegu ya utu nafsini mwa mtu. Hukabili tambio ya kila aina ya ujisadi kwa nguvu kama zile zinazoonyeshwa na ujisadi wenyewe upatikanao duniani leo hii. Mafundisho yake yamenyooka yenye nguvu na yaliyopangika vyema kana kwamba ni picha wazi ya maumbile yenyewe na nakala halisi ya kanuni za maumbile. Yafanana na juu liangazalo kwa ajili ya jicho la kiroho na vipawa vya moyo vya uelewewu.

*(Roohani Khazain Jal. 1: Braheen-e-Ahmadiyya, Uk. 81-82)*

## DINI ZA DUNIA

Miongoni mwa kanuni ambazo nimefanywa niziamini kwa dhati ipo moja ambayo imefunuliwa kwangu mahsus na Mwenyezi Mungu Mwenyewe. Kanuni yenye ni kutosema ni za asili ya ubandia zile aina za dini ambazo zilifunuliwa na Mungu kwa njia ya manabii Wake na ambazo zina alama hizi: Zimepata kukubaliwa sana katika maeneo fulani ya dunia; baada ya kushinda kila aina ya upinzani, zimepata mafanikio na ustawi mkubwa. Baada ya kudumu kwa muda mrefu, zimepata kuwa alama ya zama zao na sura ya mafanikio. Sawa na kanuni hii, dini kama hizo yamkini zilikuwa dini za kweli na bila shaka waanzilishi wao walikuwa mitume wa kweli wa Mwenyezi Mungu.

(*Rhoohani Khazain Jal. 12, Uk. 256: Tohfae Quisariya Uk. 4*)

Hii ndiyo kanuni inayopendeza zaidi na yenyе kuleta amani iliyo jiwe la msingi wa mwafaka mionganii mwa mataifa na kujenga mwenendo bora. Kanuni yatufunza kuamini ukweli wa Manabii wote popote walipopata kudhihiri iwe katika India, Uajemi au Uchina au katika nchi yo yote na ambao kwa ajili yao Mungu Amezijaza nyoyo za mamilioni ya watu kwa wingi wa hofu na heshima kubwa na kuziwezesha dini zao kusimama imara.

(*Roohani Khazain Jal. 12, Uk. 259: Tohfae Qaisariya Uk. 7*).

## HURUMA KWA WANADAMU

Kanuni tunayoifuata ni hii kwamba tuwe na huruma moyoni mwetu kwa ajili ya wanadamu wote. Kama mtu ye yote akiona nyumba ya jirani yake Baniani imepamba moto na hajitokezi kusaidia kuuzima moto, nasema kwa hakika kwamba mtu huyo si wa kwangu. Kama mfuasi wangu ye yote, baada ya kumwona mtu fulani, akijaribu kumuua Mkristo, hajitokezi kujaribu kumsaidia Mkristo yule, nasema kwa kweli kwamba mfuasi huyo hayumo kundini mwetu.

*(Roohani Khazain Jal. 12, Uk. 28, Siraj-e-Muneer Uk. 26)*

Nawatangazia Waislamu, Wakristo, Mabaniani na Waarya, kwamba katika nafsi yangu mimi sina adui duniani. Nawapenda wanadamu jinsi mama mpendwa awapendavyo wanawe; bali kwa dhati zaidi. Mimi ni adui wa itikadi mbovu pekee, zenyе kuhilikisha ukweli. Huruma kwa wanadamu wote ndio wajibu wangu. Kanuni yangu ni kutupilia mbali udanganyifu. Naukataa upagani, uovu, ubaya, dhulma na ufisadi.  
*(Roohani Khazain Jal. 17: Arbaeen sehemu 1, Uk. 2)*

## HALI YA BAADAYE YA AHMADIYYAT

Natangaza kwa matumaini na uthabiti kwamba mimi nasimama juu ya haki na kwamba kwa fadhili za Allah, nitatokea kuwa mshindi katika harakati hizi. Kadri niwezavyo kuona kwa nuru ya macho yangu yaonayo mbali naukuta ulimwengu mzima hatimaye ukifunikizwa na hatua za maendeleo ya ukweli wangu. Wakati unawadia ambapo mimi nitapata ushindi mkubwa. Hii ni kwa sababu sauti nyingine yazungumza kwa kuunga mkono nisemayo, na upo mkono mwingine unaofanya kazi ili kuupa nguvu mkono wangu. Dunia haiuoni mkono huu, lakini mimi nauona. Nafsini mwangu yajitokeza sauti ya Dhati wa mbinguni inayolipa uzima kila neno nisemalo. Mwamko na kiherehere vimezuka juu mbinguni vimeumba kutokana na fumba la udongo kiumbe mnyonge ambaye matendo yake yanaongozewa huko juu mbinguni. Wale wote ambaao, mlango wa toba bado haujafungwa kwao hivi karibuni wataona kwamba mimi si mimi binafsi. Je, yaweza kuwa macho yaonayo yasiyoweza kumtambua mtu mkweli? Je, aweza akawa hai yule ambaye haumwingii akilini wito huu wa Mbinguni?

*(Roohani Khazain Jal. 3, Uk. 403: Azalae Auham sehemu II)*

Jueni ya kwamba huu ni mti uliopandwa na Mkono wa Mungu. Hatauacha ukauke. Yeye Hatatosheka mpaka pale atakapouona umestawi na kufikia kima chake. Atahakikisha kwamba umemwagiliwa maji ya kutosha naye Atauzungushia ugo kuulinda. Hivyo Mwenyezi Mungu Atawabariki wafuasi wangu kwa mafanikio ya ajabu na ustawi. Je, hamkufanya chini juu kuupinga? Lau kama hii ingelikuwa kazi ya mwanadamu, mti huu ungelikuwa tayari umesha katwa na kuangushwa kitambo sana na haingebaki alama yake hata chembe.

*(Roohani Khazain Jal. 11, Uk. 46, Anjam-e-Atham)*

## HATIMAYE USHINDI

Watu wa ulimwenguni waweza kufikiria kwamba ni Ukristo ambao hatimaye utazagaa duniani kote, au pengine dini ya Budha ndiyo itakayoshinda mwishoni. Lakini wao bila shaka wamekosea mno katika dhana hizi zao. Kumbukeni ya kwamba hapana litendekalo hapa ardhini ila liwe limeridhiwa huko juu mbinguni. Na, ni Mungu wa mbinguni Anifunulaiye ya kwamba hatimaye ni dini ya Islam itakayozishinda nyoyo za watu.

(*Roohani Khazain Jal. 21: Braheen-e-Ahmadiyya sehemu V, Uk. 427*)

Sasa hapana Mtume na mwombezi kwa ajili ya wanadamu ila Mtukufu Mtume Muhammad, Mteule, amani na baraka za Mungu ziwe juu yake. Hivyo mwapaswa kujitahidi kuwa na upendo halisi juu ya huyu Nabii adhimu aliyetukuka wala msimuheshimu mwinginewe kuliko yeye kwa vyo vyote vile ili muweze kuhesabiwa huko mbinguni mionganini mwa wale ambao wameupata wokovu. Kumbukeni kwamba wokovu si kitu ambacho hupatikana tu baada ya kifo. Ama kusema kweli, wokovu halisi ni ule unaodhihirisha nuru yake humu humu duniani. Ni nani aliyeokolewa? Ni yeye kwa hakika, aaminiye kwamba Mwenyezi Mungu ni kweli na kwamba Mtume Mtukufu, s.a.w. ndiye mwombezi kati ya mtu na Mungu. Na zaidi ya hayo, aamini kwamba chini ya mbingu hapana Nabii sawa naye na wala hapana Kitabu chenyeh cheo sawa na Kurani Tukufu. Na aamani kwamba Mwenyezi Mungu Hakuridhia kwa mwingine ye yote kwamba aishi milele na ujumbe wake, ila huyu Nabii Mbora yuaishi milele.

(*Sajina ya Nuhu, Uk. 10*)

Kutokana na uchunguzi wa maisha ya Mtume Mtukufu itakuwa wazi kwa kila msomaji ya kwamba Mtume Mtukufu wa Islam S.A.W. katika khulka zake hakuwa kigeugeu bali nafsi yake ilikuwa safi tukufu. Daima alikuwa tayari kuutoa uhai wake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, hakuwatumania watu wala hakuwaogopa. Tumaini lake zima lilikuwa Allah. Baada ya yeye kujifanya mtumwa wa mapenzi ya Mungu kikamilifu, hakujali tena ni mikasa sampuli gani atakayokabiliana nayo

na ni mateso ya aina gani yatakayomfikia toka kwa mikono ya waabuduo masanamu kama matokeo ya yeze kuitangazia ulimwengu ujumbe wa Umoja wa Mungu.

(*Roohani Khazain Jal. 1, Braheen-e-Ahmadiyya Uk. 111*)

Je, halikuwa jambo la ajabu sana kupata kutokea kwamba katika zama ambapo mataifa yote makubwa yalikuwa na uwezo mkubwa wa mali, kijeshi na elimu, yatima masikini, asokuwa na uwezo, mnyonge, asojuua kusoma wala kuandika na bila msaada wo wote, akaleta mafundisho bora ambayo, kwa hoja zake zenye kukolea na mathibitisho yake yasosutika, yakamnyamazisha kila mpinzani? Halikhadhalika, mafundisho hayo pia yalifichua makosa na ubovu wa wanazuoni ambaa chini ya gamba la udanganyifu wao walijigamba kuwa mabingwa wa filosofia na wataalamu wenye elimu. Licha ya yeze kuwa maskini na mnyonge akapata nguvu nyingi na akawavua taji wafalme wakubwa wakubwa na kutawalisha maskini pahali pao. Kama haya yote hayakutoka kwa Allah, basi ilikuwaje? Kushinda ulimwengu mzima kisha kuupita wote katika nyanja za hekima, elimu na uwezo, je haya yote yanaweza yakapatikana bila ya msaada wa Allah?

(*Roohani Khazain Jal. 1, Braheen-e-Ahmadiyya*)

Hebu tazama: Jinsi Mtume Mtukufu wa Islam alivyodumu kuwa thabiti na imara katika madai yake ya utume tangu mwanzo hadi mwisho licha ya kukabiliwa na maelfu ya hatari na makundi ya maadui na wapinzani wenye vitisho. Kwa miaka mingi yeze alivumilia shida na mateso yaliyoongezeka siku baada ya siku; kutosha kumvunja mtu moyo. Isingeliwezekana kwa mtu mwenye tamaa za kidunia kuonyesha uthabiti na uvumulivu wa muda mrefu kama huo. Si hayo tu, bali kwa madai yake ya utume, yeze pia akapoteza hata ule msaada aliokuwa akiupata hapo awali. Gharama aliyotakiwa kulipia dai lake moja ilikuwa kukabiliana na mamia ya maelfu ya ushindani na kujitakia maelfu ya mikasa. Aliihama nchi yake huku akizozwa kwa shabaha ya kuuawa; nyumba na vyombo vyake viliharibiwa, majoribio kadha ya kumpa sumu pia yalifanywa. Wale waliokuwa wakimpenda sasa wakaanza kumhasimu. Marafiki wakamgeuka. Kwa ajili ya zama zilizoonekana kuwa za milele yeze akavumilia dhiki asizoweza kuvumilia hata kidogo mwongo na mlaghai.

(Roohani Khazain Jal. 1: Braheen-e-Ahmadiyya Uk. 108)

Nabii Daudi a.s. alithibitisha ukuu na utukufu wa Mtume Mtukufu S.A.W. alipotamka akisema katika Zaburi 45:

Wewe u mzuri sana kuliko wanadamu,  
Neema imemiminwa midomoni mwako,  
Kwa hivyo Mungu amekubariki hata milele.

Jifunge upanga wako pajani, wewe uliye hodari,  
Utukufu ni wako na fahari ni yako.

Katika fahari yako usitawi uendelee  
Kwa ajili ya kweli na upole na haki  
Na mkono wako wa kuume  
Utakufundisha mambo yakutisha.

(Roohani Khazain Jal. 2: Surma Chashm-e-Arya Uk. 232-34)

Baraka Zako zisizo kikomo ziwe juu ya Mustafa,  
E Mwenyezi Mungu,  
Hakika, toka kwake twapata nuru Yako.

Roho yangu imefungamanishwa daima na roho ya Muhammad.  
Niliunywesha moyo wangu maridhawa toka kikombe cha upendo huu.

Yule kiongozi wetu inakotoka nuru yote, jina lake ni Muhammad,  
Ndiye aliyeuvama moyo wangu.

Manabii wote ni watakatifu, mmoja kuliko mwingine.  
Toka kwa Mungu juu yeye ndiye mbora wa viumbe.

Mbora kuliko wote wa awali,  
yuwang 'aa kama mwezi kwa utukufu.  
Kila jicho kamtazama yeye.  
Naam, na ndiye mwezi mzima uangazao giza.

Wale wa kabla yake walifika nusu ya njia,  
yeye ndiye aliyehitimisha mafanikio salama salimini.  
Laiti ningalikufa kwa ajili yake,  
yeye pekee ndiye kiongozi bora.

Yule Mpendwa asozingwa na mazingara,  
Yule kipenzi wa vina vya moyo wangu,  
Alidhihirishwa kwetu naye (Muhammad),  
Mwongozo wake ni wa kipekee.

Leo hii yeye yu mfalme wa Ufalme wa kiroho,  
taji la Manabii wote.  
Kusema kwamba yeye yu myofu na astahiliye amana  
ni pongezi stahilifu kwake.

Jicho lake laona mbali,  
moyo wake daima wamkaribia Mungu.  
Akiunyanya mwenge,  
yeye ndiye chanzo cha nuru.

Yeye ndiye aliyetuonyesha hekima ya ndani ya imani;  
Mfalme bora, mgawaji mkarimu wa hazina.

Naishi na kufa kwa ajili ya nuru ile, mimi ni wake yeye pekee.  
Yeye pekee ndiye wa kuthaminika nami wala sijali; huu ni uamuzi wa  
mwisho.

Siwezi kumpata aliye bora kuliko yeye duniani.  
Kwa kweli, nimeunasua moyo wangu toka kwa kamato la wengineo.

Adhma ya Mungu yadhihirika katika  
utawa wako ewe mpPENDWA wangu.  
Nimemfanya Yeye kuwa wangu  
kwa kukufanya wewe kuwa wangu.

Baada ya kugusa pindo za vazi Lako,  
E Mwenyezi Mungu,

mtu huokolewa kutokana na nira  
ya uzuri wa vinginevyo.

Hakika, mimi nasujudu mbele ya kizingiti Chako pekee.  
E wangu Mpendwa naapa kwa Umoja Wako.  
Katika mapenzi yangu Kwako  
Mimi binafsi nimejisahau.

Wallahi, matamano mingine yote  
yametoweka moyoni mwangu  
angu uso Wako uliponiangazia.

Ni kwa sababu yako kwamba tulikuwa umati bora,  
E Nabii wa Mungu uliye Mbora wa Manabii wote  
Kadri ulivyowatangulia wengine,  
nasi pia tukasonga mbele.

Achilia mbali wanadamu wengine,  
hata Malaika wa Mbinguni wafanya vivyo hivyo  
na kuijunga nami katika  
kuhimidia utukufu Wako.

Isingeliwezekana kwangu mimi kuipata neema hii kama nisingelifuata nyayo za Bwana kiongozi wangu, fahari ya Manabii wote, Mbora wa wanadamu, Muhammad, Mteule, amani na baraka za Mungu ziwe juu yake. Mafanikio yo yote nimeyapata kwa kumfuata yeye, nami najua kutokana na uzoefu uliohakiki, ya kwamba hapana awezaye kumpata Mwenyezi Mungu na kupata elimu ya ndani ya njia Zake bila kumfuata Nabii yule, amani na baraka za Mungu ziwe juu yake. Sasa, hebu pia nitoboe ya kwamba kitu cha kwanza unachozawadiwa, baada ya kusalimu kabisa amri na mafundisho ya Mtume Mtukufu Muhammad, ni hiki kwamba unapewa moyo mpya ambao daima wavutiwa na wema, yaani, moyo usiovutiwa na dunia hii, na badala yake unaanza kutamani raha ya milele ya mbinguni. Baada ya kutimiziwa tamanio hili, moyo huu sasa huwa tayari kupokea ule upendo nadhifu, ule mtimilifu upendo wa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu ya wewe kumtii yeye (Mtume Mtukufu) baraka hizo zote wewe hupewa kama turathi yake ya kiroho.

(*Haqeeatul Wahyi* Uk. 64).